

Habari kuhusu unachofanya baada ya kupimwa korona

KAA NYUMBANI MPAKA MAJIBU YAPATIKANE. Kwa muda wa siku 1-2 utaweza kupata majibu. Hautapokea taarifa/habari yoyote kwamba matokeo/majibu yako tayari. Ingia kwa tovuti/kwenye www.helsenorge.no ili usome majibu yako mwenyewe na watoto wako. Ikiwa hauna uwezo wa kuingia kwenye tovuti helsenorge.no, ni lazima uwasiliane na daktari wako ili upata matokeo/majibu ya vipimo hivyo. Unaweza pia kupiga simu ya korona kwa nambari hii 55 56 77 00

KIPIMO CHANYA - POSITIV: KIPIMO KINACHOONYESHA MAAMBUKIZI YA KORONA

Kila mtu aliye na kipimo kinachoonyesha maambukizo ya korona ataitwa wala atapokea ujumbe wa SMS kutoka kituo cha afya ya dharura ya Bergen-legevakten.

Ikiwa majibu yanaonyesha maambukizoni ya korona ni lazima:

- ukaae nyumbani
- ukaae mbali na wale unaoishi nao na ikiwezekana utumiye chumba chako na bafu peke yako
- uhakikishe kuwa mikono, nyuso/surface na mazingira ni safi

Ni lazima wengine katika familia watenganishwe-karantini. Ni lazima utengwe hadi siku 10 baada ya dalili/symptomes za korona kuanza, na ni lazima usiwe na homa kwa masaa 24 yaliyopita.

Chunguza ni watu gani uliowasiliana / ulikutanana/ ulishirikia nao tangu wakati ulipougua/ulipo gongjwa na siku 2 kabla. Wafahamishwe/ wajulishwe kuwa inawezekana wakawa wameambukizwa na ni lazima watenganishwe. Ofisi ya Kudhibiti Maambukizo Bergen itawasiliana na wewe, ili kupatia habari zaidi.

Unaweza kusoma habari zaidi juu ya sheria za kutenganisha nyumbani na karantini katika tovuti

www.bergen.kommune.no/koronavirus na www.fhi.no

KIPIMO HASI - NEGATIV: KIPIMO KINACHOONYESHA KAMA HAKUNA MAAMBUKIZI NA KORONA

Kama/ Ikiwa matokeo/majibu yanaonyesha "Haijagunduliwa/kuambukiziwa wala haija onyesha kitu" kwenye tovuti ya www.helsenorge.no, inamaanisha kama hakuna virusi vya korona vilivyopatikana wakati wa kupimwa. Ikiwa/uko katika karantini, ni muhimu/lazima uendeleye kukaa kwa karantini hadi siku 10 zimalizike zote. Virusi hivi inaitajia muda fulani wa kuisha nguvu/ muda wa incubation". Unaweza kuwa kwa kweli umeambukizwa ingawa vipimo haithibitishi kwamba umeambukizwa/ hata kama vipimo hazionyeshi kama umeambukiziwa.

Ikiwa/kama una "homa " ya kawaida au una ugonjwa wa matatizo ya kupumua, bila kutengwa, ni lazima ukaae nyumbani hadi uwe katika hali nzuri ya kiafya. Wafanyakazi wa afya ambao wamekuwa na dalili/symptomes za korona wanapashwa kuwasiliana na mwajiri/bosi wao kabla ya kurudi kazini.

Ni muhimu ujuwe ni ushauri gani ambayo inakuhusu kwenye tovuti www.fhi.no.

Ikiwa unakuwa na dalili/symptomes wakati unaosubiri matokeo/majibu ya kupimwa au uko katika karantini, labda umeambukizwa na ni lazima utenganishwe mara moja. Ni lazima uwajulishe wengine nyumbani mwako mara moja na wengine ambao una uhusiano wa karibu ili wajitenge.

Tafuta msaada ikiwa una ugonjwa mahututi/sana. Wasiliana/ongea na daktari wako au kituo cha afya dharura kwa nambari 116 117. Ikiwa una dalili/symptomes za ugonjwa wa dharura, wasiliana na 113. Zingatia sana kuongezeka kwa kupumua. Kumbuka kuripoti kupitia kwa simu ikiwa umetengwa au uko kwa karantini kwa sababu ya Covid-19.



BERGEN
KOMMUNE

BERGEN LEGEVAKT